

HALI YA UMEME VIJIJINI

Katika Mkoa wa Njombe Miradi ya Umeme kupitia mfuko wa Millennia unatekelezwa katika wilaya za Wanging'ombe na Makete. Kazi inahusisha Ujenzi wa njia za Umeme na ufungaji wa "Transformer" maeneo ya Hospitali ya Ikonda na Chuo cha walimu Tandala, Majengo Mapya Makambako na eneo la Barabara ya Mbeya katika Mji wa Makambako. Miradi hii katika Mkoa wa Njombe na Iringa itagharimu jumla ya shilingi 24,000,000,000.

Pia kuna Mradi wa umeme wa Makambako- Songea unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la SWEDEN (SIDA) na utahusisha Wilaya za Wanging'ombe, Njombe, na Ludewa na unatarajiwa kugharimu Shilingi 29,600,000,000 Mchakato wa kuwapata wakandarasi unaendelea.

Hali ya Utekelezaji wa mradi huu unaendelea kutekelezwa kama ifuatavyo: -

- Mradi wa Utiga katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe upo kwenye "REA Phase 1" na utagharimu Shilingi 93,331,126.44. Katika awamu ya Pili (REA phase II). Miradi mbalimbali katika Halmashauri za Makete, Njombe na Wanging'ombe yenye thamani ya shilingi 11,611,038.80 itajengwa.

Aidha Kwa Mwaka wa fedha 2013/2014 TANESCO wametekeliza miradi ifuatayo

- Luana – Ludewa,
- Ludewa, Nindi, Ntumbati na Lupingu.